



TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT MUJIBU WA SHERIA MWAKA 2023

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), linawaita Vijana wote waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2023 kutoka Shule zote za Tanzania Bara kuhudhuria Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2023.

Sanjari na wito huo, JKT limewapangia makambi watakayo kwenda kupatiwa Mafunzo na wanatakiwa kuripoti makambini kuanzia tarehe 01 Juni hadi 11 Juni 2023.

Vijana hao wamepangwa katika Kambi za JKT Rwamkoma - Mara, JKT Msange - Tabora, JKT Ruvu - Pwani, JKT Mpwapwa, Makutupora JKT - Dodoma, JKT Mafinga - Iringa, JKT Mlale - Ruvuma, JKT Mgambo na JKT Maramba -Tanga, JKT Makuyuni - Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa na JKT Mtabila - Kigoma, JKT Itaka - Songwe, JKT Luwa na JKT Milundikwa - Rukwa, JKT Nachingwea - Lindi, JKT Kibiti- Pwani na Oljoro JKT- Arusha.


Wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho (*Physical Disabilities*) waripoti katika Kambi ya Ruvu JKT iliyopo Mlandizi Mkoani Pwani ambayo ina miundombinu ya kuhudumia watu wa jamii hiyo.

Aidha JKT linawataka vijana hao kuripoti wakiwa na vifaa vifuatavyo.

1. Bukta ya rangi ya 'Dark Blue' yenye mpira kiunoni, iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini, isiyo na zipu.
2. T-shirt ya rangi ya kijani (Green Vest)
3. Raba za michezo zenye rangi ya kijani au blue.
4. Shuka mbili za kulalia zenye rangi ya blue bahari.
5. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
6. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenye baridi.
7. Track suit ya rangi ya kijani au blue.
8. Nyaraka zote zinazohitajika katika Udahili wa Kujiunga na Elimu ya Juu, zikiwemo cheti vya Kuzaliwa, Vyeti vya Kuhitimu kidato cha Nne nk.
9. Nauli ya kwenda makambini na kurudi nyumbani.

Orodha kamili ya majina ya vijana hao, Makambi ya JKT waliyopangiwa na maeneo Makambi hayo yalipo na vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, Inapatikana katika tovuti ya JKT ambayo ni www.jkt.go.tz

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, Anawakaribisha vijana wote waliohitimu kidato cha sita mwaka 2023 kuungana na Vijana wenzao ili kujengewa Uzalendo, Umoja wa Kitaifa, kufundishwa stadi za kazi, Stadi za Maisha na Utayari wa Kulijenga na Kulitumikia Taifa lao.



Imetolewa na:

**Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,
Makao Makuu ya JKT,
Tarehe 25 May 2023.**